**HOTUBA YA MHE. JERRY WILLIAM SILAA (MB), WAZIRI WA MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI, KATIKA HAFLA YA UZINDUZI WA BODI YA WAKURUGENZI WA MFUKO WA MAWASILIANO KWA WOTE (UCSAF)**

**UKUMBI WA MIKUTANO – JENGO LA UCSAF, DODOMA**
**TAREHE 4 FEBRUARI 2025**

**Bw. Mohammed Khamis Abdulla, Katibu Mkuu, Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari;**
**Bw. Nicholas Mkapa, Naibu Katibu Mkuu, Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari;**

**Mhe. Balozi Valentino Longino Mlowola, Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi ya UCSAF;**
**Waurugenzi kutoka Wizarani;**

**Wajumbe wa Bodi ya UCSAF;**

**Mhandisi. Peter Mwasalyanda, Mtendaji Mkuu na Katibu wa Bodi ya wakurugenzi ya UCSAF:**

**Menejimenti na Wafanyakazi wa Wizara na UCSAF mliopo;**

**Waandishi wa Habari;**

**Mabibi na Mabwana.**

Awali ya yote napenda kumshukuru Mwenyenzi MUNGU kwa kutuwezesha sote kuwa salama na kukutana leo hii hapa kushuhudia uzinduzi wa Bodi hii. Lakini nitumie nafasi hii pia kuwapongeza Mwenyekiti, Bodi na Menejimenti kwa namna ambavyo mmeendelea kutimiza majukumu yenu kwa tija na weledi.

***Ndugu Mwenyekiti na Wajumbe wa Bodi,***

Kama ambavyo, Katibu Mkuu ameeleza kuwa Taasisi hii ni nyeti na ya kimkakati hivyo mmeaminiwa na kupewa jukumu kubwa hivyo lazima muilinde Imani hiyo kwa Vitendo. Hivyo nitumie nafasi hii kuwapongeza nyote kwa kuteuliwa kwenye nafasi zenu.

***Ndugu Mwenyekiti na Wajumbe wa Bodi,***

Kwa kipindi hiki kama Mfuko umepewa jukumu kubwa na la kimkakati ambalo lilishuhudiwa na Mheshimiwa Rais, wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambapo mnatekeleza mradi ambao unatawezesha Taifa letu kupiga hatua Zaidi katika kuchochea ukuaji wa uchumi wa Kidijitali, hivyo nitumie nafasi hii kuwaambia masuala yafuatayo;

i. Kumuelekeza Mwenyekiti na wajumbe kuhakikisha kuwa utekelezaji wa mradi wa ujenzi wa minara 758 unakamilika mapema kwani, nimejulishwa kuwa hadi kufikia tarehe 31

Januari 2025 minara iliyowashwa ni asilimia hamsini (yaani minara 380). Kwa kuangalia muda uliobaki wa miezi minne (4), inabidi mfanye jitihada kubwa sana kuwasimamia watoa huduma ili kukamilisha mradi huu kwa wakati. Hivyo, ninapenda kuchukua fursa hii kuwaelekeza kuwa ufuatiliaji wa utekelezaji wa mradi huu upewe kipaumbele namba moja katika majukumu yenu.

ii. Hakikisheni kuwa hali ya mawasiliano mipakani inaboreshwa, shirikianeni na TCRA kuona namna bora ya kukabiliana na changamoto za hali ya Mawasiliano mipakani;

iii. Muanze kuangalia namna bora ya kiteknolojia ya kusimamia au kufuatilia minara inayojengwa na watoa huduma inafanya kazi wakati wote;

iv. Muone namna bora ya kushirikiana na wadau wengine ili kuhakikisha utoaji wa vifaa vya TEHAMA unakuwa wa tija na kuhakikisha matokeo chanya yanaonekana;

v. Kuimarisha usimamizi wa Ofisi za Kanda ili ziweze kuwasaidia katika kupunguza malalamiko au changamoto zinanazojitokeza kwa wakati, hakikisheni zinakuwa na wataalamu wa kutosha lakini wakafanye kazi kwa ukaribu

na Halmashauri na viongozi wa mikoa na hii itarahisha utekelezaji wa majukumu yenu na hivyo kero kwa wananchi zitakuwa zinafanyiwa kazi kwa ukaribu;

vi. Nafahamu kwamba kwa muda mrefu UCSAF imekuwa ikitumia rasilimali nyingi zaidi kwenye miradi ya huduma za mawasiliano ya simu na asilimia ndogo sana imekuwa ikielekezwa kwenye sekta ndogo **(sub-sector)** nyingine za mawasiliano (hapa namaanisha posta, utangazaji na TEHAMA), hivyo ni rai yangu kwamba na hizo sub-sector nyingine muone namna za kuangaliwa;

**Ndugu Mwenyekiti na Wajumbe wa Bodi;**

Ninapenda kuwakumbusha kutimiza vyema majukumu yenu kama yalivyoainishwa kwenye Sheria ya Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote, Sura ya 422 pia kwa kuzingatia Nyaraka na Miongozo ya Serikali hususan zinazotolewa na Msajili wa Hazina kuhusu uendeshaji wa shughuli za Bodi, Mwongozo ya Bodi (Board Charter) na Miiko na Maadili ya Utendaji kazi.

***Ndugu Mwenyekiti na Wajumbe wa Bodi,***

Ninapomalizia hotuba yangu, nirudie kuwapongeza tena Mwenyekiti na Wajumbe wa Bodi kwa kuteuliwa kuwa katika Bodi hii. Ni matumaini yangu kwamba tutashirikiana vizuri katika sekta yetu ya mawasiliano na kila mmoja wenu atatekeleza wajibu wake ipasavyo. Niwaombe muoneshe mfano mzuri katika utendaji wenu ili tuweze kufanikisha malengo yetu ya pamoja ya kuhakikisha huduma za mawasiliano zinafika kote nchini.

**Ndugu Mwenyekiti na Wajumbe wa Bodi,**

Baada ya kusema haya, ninapenda kutamka kuwa **Bodi ya Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote (UCSAF) imezinduliwa rasmi,** na sasa nipo tayari kuwakabidhi Mwenyekiti wa Bodi na Wajumbe wa Bodi vitendea kazi kwa ajili ya kutekeleza majukumu yenu kikamilifu.

**ASANTENI KWA KUNISIKILIZA**